


dawa za kilimo, chanjo, vyakula vya mifugo n.k; (3) Malipo ya malazi nje ya kituo cha kazi, malipo ya ziada ya muda wa kazi na malipo mengine kwa wafanyakazi wa serikali za mitaa; (4) nishati na usafiri; (5) Mahitaji ya ofisi na matumizi kama watoaji huduma za kompyuta, nukushi na nakala, ushauri na kazi za mikataba; (6) Nishati na usafiri kama mafuta ya dizeli, petroli, tiketi za ndege, ukodishaji wa magari, usafiri wa ardhi n.k; (7) Mafunzo na machapisho inajumuisha vitu kama gharama za mafunzo, machapisho, vifaaa vya mkutano, n.k; (8) Chakula na viburudisho; (9) Ukarabati na ugavi kwa ujumla.

Ni wazi kwamba kiwango kikubwa cha fedha hutumiwa kwa gharama ambazo si za moja kwa moja, ambapo fedha za msaada zinazopelekwa kwenye maendeleo ya kilimo wilayani (DADG) hazitoshi kuleta mabadiliko kwenye sekta. Uchambuzi zaidi umeonyesha kwamba mikoa maskini<sup>3</sup> zaidi ya Tanzania hupokea asilimia 15.1 ya bajeti, wakati mikoa yenye umaskini wa wastani na ile yenye unafuu kiuchumi hupata kati ya 44.3% na 40.4%. Ingawa mgawanyo huo unaweza kuchochewa na umuhimu wa mkoa husika na uwezo katika kilimo, lakini kama mgawanyo huu hautaratibiwa vizuri basi matokeo yake ni kutokuwepo kwa usawa miongoni mwa mikoa.

Mlinganisho wa mwelekeo wa makadirio ya bajeti na bajeti halisi ya sekta ya kilimo



Mchoro huu unaonyesha pengo kubwa kati ya makisio na tarakimu za mgawanyo halisi kwenye sekta ya kilimo. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2011/12, tofauti/pengo ni zaidi ya asilimia 40. Tafsiri yake ni kwamba kutakuwa na upungufu ambao hautaendana na ubora kwa ujumla.

Wakati sekta hii ikiendelea kukua kwa zaidi ya miongo miwili, Tanzania haijaweza kufikia Azimio la Maputo la 2003 lililopitishwa na Umoja wa Afrika ambalo lilipendekeza kwamba asilimia 10 ya bajeti yote ya taifa ielekezwe kwenye kilimo.

## Hitimisho na Mapendekezo

- Mikoa maskini kupatiwa msaada kwa kiwango cha chini - inamaanisha kwamba kama mipango haitawekwa wazi na kusimamiwa kwa umakini, hakutakuwa na usawa na kuondoa umaskini kwa mikoa husika;
- Kiwango cha uwekezaji kwa Tanzania hakitoshi kuleta mapinduzi ya kilimo kama ilivyopendekezwa kwenye Azimio la Maputo (2003) la Umoja wa Afrika;
- Lengo la serikali la kuwekeza kwenye maendeleo ya kilimo kwa asilimia 65 liliwekwa kando na utaratibu na mfumo wa LGA na muda wa kutoa mikopo ikimaanisha kwamba asilimia kubwa ya fedha za maendeleo hutumika kwenye gharama nyingine zisizo za moja kwa moja badala ya kuwasaidia wakulima;
- Serikali kupitia Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) lazima iweke mfumo na taratibu ambazo zitahakikisha masharti ya dhamana hayawakwamishi wakulima wadogo kupata mikopo;
- Ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Kilimo Kwanza, LGAs zinapaswa kutenga kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwenye vyanzo vyake ili kuchochea shughuli za kilimo;
- Ili kuweka uwiano sawa kati ya mikoa, iko haja ya kupima kiwango cha umasikini kwenye mikoa husika wakati wa kugawanya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PMORALG);
- Kuwepo na mfumo mmoja wa kuandaa bajeti na ufuatwe na serikali zote za mitaa (LGAs) ili kurahisisha ufuatiliaji wa bajeti;
- Taarifa za kina za mgawanyo wa bajeti kuanzia serikali za mitaa hadi taifa ziwekwe wazi na zipatikane kwa wadau wote wenye nia ya kufuatilia bajeti.

Uchambuzi huu wa sera umeandaliwa na ANSAF, mwanachama wa Kikundi Kazi cha Bajeti cha Policy Forum.

ANSAF ni mtandao wa mashirika ya hiyari CSOs, kampuni (za ndani ya nchi na kimataifa) na wakulima wadogo wanaofanya kazi ya kukuza uelewa kupitia mafunzo, kubadilishana uzoefu, kuongeza uwekezaji katika kilimo na kuibua mijadala ya sera na watoa maamuzi.

Policy Forum ni mtandao unaoshirikisha zaidi ya mashirika ya hiyari 100, yanayoshughulikia kupunguza umasikini, kuleta usawa na demokrasia, utawala bora na uwajibikaji.